

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA

13 JUNI, 2024



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA TAREHE 13 JUNI, 2024

**I. DUA:**

**II. TAARIFA YA SPIKA:**

**III. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Mhe. Khamis Yussuf Mussa

**IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## **WAZIRI WA FEDHA:**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (*Monetary Policy Statement*) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## **V. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

## **VI. MASWALI YA KAWAIDA:**

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **606. MHESHIMIWA EDWARD OLELEKAITA KISAU (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha kuboresha miundombinu ya Minada ya Kibaya, Dosidosi na Suuyu.

#### **607. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza posho kwa Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Madiwani.

**608. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kujenga madaraja yaliyoharibika katika Jimbo la Kwela.

**WIZARA YA NISHATI:**

**609. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wafanyabiashara wanaopata hasara kutokana na kukatika kwa umeme pasipo mpangilio - Segerea.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**610. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA Wilayani Mbanga.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **611. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Barabara ya Holili hadi Tarakea Wilayani Rombo.

### **612. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Dimani hadi Mloka kwa kiwango cha lami.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **613. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Wanajeshi Wastaafu waliopigana Vita ya Kagera watalipwa mafao yao.

## VII. HOJA ZA SERIKALI:

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SAA 10:00 ALASIRI**

### **WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA  
13 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**